# Itifaki ya Kulinda Aina Mpya za Mimea/Mbegu kwa Nchi za SADC:

## Mpango wa kukubalika kwa UPOV 1991 barani Afrika




MUKHTASARI


african centre for biodiversity
www.acbio.org.za

September 2018

# TOC


**VIfupisho** 3

**Matumizi ya maneno** 4

**Utangulizi na Historia Fupi** 4

**Wasiwasi kuhusu Itifaki ya kulinda aina ya mbegu kwa nchi za SADC** 5

Utaratibu wa kulinda aina ya mbegu chini ya mamlaka moja 5

Kutokuwepo kwa Mfumo wa Kipekee wa kulinda aina ya mimea 6

Kulindwa kwa (jenera na spishi)/ aina yote ya mimea 6

Kigezo cha NDUS 6

Kubaini uasilia wa aina ya mimea 6

Wigo wa haki za wagunduzi 7

Misamaha katika haki za wagunduzi na fursa kufanikisha haki za wakulima 8

**Hitimisho na Mapendekezo** 9

Kuzingatia tofauti baina ya Itifaki za Ulinzi wa mimea za SADC na Arusha 9

Mapendekezo kwa nchi wanachama wa SADC 10

**Kiambatisho** 12

Mnamo Aprili 7, 2015 Kituo cha Afrika cha Usalama wa Kibaiolojia kilibadilisha jina lake rasmi na kuitwa Kituo cha Afrika cha Bioanuwai (ACB). Mabadiliko haya ya jina yalikubaliwa kupitia mashauriano ndani ya ACB ili yaakisi kupanuka kwa wigo wa kazi yetu katika kipindi cha miaka michache iliyopita. Machapisho yote ya Kituo cha Afrika cha Bioanuwai kabla ya tarehe hii yatabaki chini ya jina la zamani la Kituo cha Afrika cha Usalama wa Kibaiolojia, na kinapaswa kuendelea kufanyiwa marejeo kama hivyo.

Dhamira yetu imeeendelea kuwa kubomoa ukosefu wa usawa katika mifumo ya chakula na kilimo barani Afrika na tunaamini yetu katika haki za watu za kupata chakula chenye lishe na stahiki kitamaduni, kilichozalishwa kupitia njia zilizo sahihi kiekolojia na endelevu, na haki yao ya kuainisha mifumo yao wenyewe ya chakula na kilimo.

© Kituo cha Afrika cha Bioanuwai

www.acbio.org.za
S.L.P. 29170, Melville 2109, Johannesburg, Afrika Kusini. Simu: +27 (0)11 486 1156

Picha ya Jalada: Helen Day
Copy editor: Inga Norenius
Mhariri nakala: Inga Norenius
Ubunifu na mpangilio: Adam Rumball, Sharkbuoys Designs, Johannesburg

Ripoti hii ilifanyiwa utafiti na kuandikwa na Sabrina Masinjila na Mariam Mayet

## Shukrani

Kituo cha Afrika cha Bioanuwai kinatoa shukrani zake kwa Bi. Sangeeta Shashikant kutoka Third World Network (TWN) kwa mchango wake mkubwa katika kujenga uwezo wa Kituo cha ACB kuhusu sheria za kulinda aina za mbegu.

Kituo cha Afrika cha Bioanuwai kinatoa shukrani kwa mchango wa Shirika la Ushirikiano wa Maendeleo la Uswisi (SDC). Hata hivyo, maoni na mawazo yaliyomo kwenye ripoti hii si lazima yawe ya SDC.

# VIfupisho

| | |
|---|---|
| ARIPO | Shirika la Kanda ya Afrika la Hatimiliki za Kitaalamu |
| ACB | Kituo cha Afrika cha Bioanuwai |
| CBD | Mkataba wa Bioanuwai |
| CSOs | asasi za kiraia |
| EU | Umoja wa Ulaya |
| ITPGRFA | Mkataba wa Kimataifa wa Ulinzi wa Rasilimali za Kijenetiki za Mimea kwa Chakula na Kilimo |
| NDUS | mpya, upekee, mfanano na uthabiti |
| LDC | nchi yenye maendeleo duni |
| PBR | haki za wagunduzi wa mimea |
| PVP | ulinzi wa anina za mimea |
| SADC | Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika |
| TRIPS | Vipengele vinavyohusiana na Biashara na Haki Miliki za Kitaalamu |
| UPOV | Muungano wa Kimataifa wa Kulina Aina Mpya za Mimea |
| WTO | Shirika la Biashara Duniani |

## Matumizi ya maneno

**Ulinzi wa Aina za Mimea**
Pia hujulikana kama Haki za Wagunduzi wa Mimea. Huu ni ulinzi wa hakimiliki za kitaalamu zinazotolewa kwa mmiliki juu ya aina mpya ya mmea. Ulinzi wa aina ya mimea na Haki za wagunduzi wa mimea mara nyingi hutumika kwa kubadilishana.

**Itifaki ya Arusha ya Ulinzi wa aina mpya ya mimea**
Itifaki ya Arusha ya Ulinzi wa aina mpya ya mimea ni itifaki iliyotayarishwa chini ya Shirika la Kanda ya Afrika la Hatimiliki za Kitaalamu (ARIPO)[1]. ARIPO ni shirika la kiserikali ambalo linawezesha ushirikiano miongoni mwa nchi wanachama katika masuala ya hakimiliki za kitaalamu. Kwa sasa kuna nchi 19 ambazo ni wanachama wa ARIPO. Jina la Itifaki ya 'Arusha' linaonyesha mahali ambapo Itifaki iliridhiwa na nchi wanachama nchini Tanzania, mwaka 2015. Majina ya 'ARIPO' na 'Arusha' katika kuitambulisha Itifaki ya Ulinzi wa aina mpya ya mimea chini ya ARIPO mara nyingi hutumika kwa kubadilishana.

**Mifumo ya mbegu inayosimamiwa na mkulima /Mifumo ya mbegu ya mkulima**
Pia hujulikana kama 'mfumo wa mbegu usio rasmi', dhana tusiokubaliana nayo. Ni mazoea ya kihistoria na kitamaduni ya wakulima kuhusu usimamizi wa mbegu na vipandikizi, ikiwa pamoja na uhifadhi wa mbegu shambani, kuendeleza na kuchagua uanuwai wa mbegu, kuhifadhi, matumizi ya kurudia, kubadilishana na kuuziana mbegu miongoni mwa familia, majirani na jamii.

## Utangulizi na Historia Fupi

Itifaki ya kulinda aina ya mimea kwa nchi za SADC ni mfumo wa kikanda wa kulinda aina za mime uliotayarishwa chini ya mamlaka ya SADC[2]. Kwa kawaida huitwa 'Itifaki ya Ulinzi wa aina mpya ya mimea kwa nchi za SADC' au 'Itifaki'). Itifaki hii iliridhiwa katika Kilele cha Mkutano wa 37 wa Kawaida wa Wakuu wa Nchi na Serikali za SADC jijini Pretoria, Afrika Kusini, mnamo Agosti 19 na 20, 2017. Wakati wa kuandika, ilikuwa tayari imetiwa saini na nchi za Angola, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Eswatini,[3] Zambia, Lesotho na Namibia.

Tofauti na mwenzake, Itifaki ya Arusha ya kulinda aina mpya ya mimea,[4] hakuna kanuni ambazo zimesha tengenezwa za kutekeleza Itifaki ya SADC. Itifaki ya kulinda aina mpya ya mimea kwa nchi za SADC tunaweza kusema haijakamilika na haitekelezeki hadi pale kanuni hizo pia zitakuwa zimeridhiwa rasmi.

Utaratibu huu unatokana na mfumo wa kikanda ulio na mamlaka kutoka sehemu moja, ambapo mfumo huo huo unaridhiwa na wanachama wa jumuiya ya kanda ya uchumi. Lengo ni kuendeleza kwa kasi biashara na uzalishaji wa aina za mbegu zilizozalishwa kibiashara kwa faida ya kampuni za mbegu/kilimo-biashara. Itifaki hii inatokana na Muungano wa Kimataifa wa Kulinda Aina Mpya za Mimea (UPOV[5] 1991), ambao ni utaratibu wa kisheria wa kimataifa ulio kandamizi na usionyumbuka. UPOV 1991 unaotoa hakimiliki za kitaaluma zenye nguvu sana kwa wagunduzi wa kibiashara, na kudhoofisha haki za wakulima. Itifaki ya kulinda aina ya mimea kwa nchi za SADC ni sehemu ya muundo wa kisheria na kitaasisi uliobuniwa kuwezesha mageuzi ya kilimo cha Kiafrika kutoka misingi ya mkulima mdogo kwenda kwenye mfumo wa Mapinduzi ya

1. Botswana, Gambia, Kenya, Lesotho, Malawi, Msumbiji, Namibia, Sierra Leone, Liberia, Rwanda, São Tomé na Príncipe, Eswatini, Tanzania, Uganda, Zambia na Zimbabwe
2. Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC) ni Jumuiya ya Uchumi ya Kanda yenye nchi wanachama 16 za: Angola, Botswana, Comoro, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Eswatini, Lesotho, Madagascar, Malawi, Mauritius, Mozambique, Namibia, Seychelles, South Africa, Tanzania, Zambia na Zimbabwe.
3. Huko nyuma ilikuwa inajulikana kama Ufalme wa Swaziland.
4. Tembelea ACB (2018b). https://acbio.org.za/sites/default/files/documents/The%20Arusha%20Protocol%20and%20Regulations_Institutionalising%20UPOV%201991%20in%20African%20seed%20systems%20and%20laws.pdf Tafadhali rejea kwenye orodha ya marejeo ya ripoti kamili
5. UPOV ni kifupisho cha Kifaransa kwa Muungano wa Kimataifa wa Kulinda Aina Mpya za Mimea. Ilitayarishwa na nchi za viwanda kushughulikia mahitaji yao ya uzalishaji na kuendeleza mimea.

Kijani/kilimo cha viwanda ambao hauna usawa na usio endelevu kiekolojia. Kama utaratibu wa kulinda aina ya mimea unaotokana na UPOV 1991, unadhoofisha haki za wakulima kwa uhuru wa kuhifadhi, kutumia, kubadilishana na kuuza mbegu zote za shambani, huminya ubunifu, hupandisha gharama za pembejeo kwa wakulima na huruhusu wagunduzi wa kibiashara kumiliki na kubinafsisha maarifa ya kihistoria ya jamii na michakato ya asili ya kiekolojia iliyojikita kwenye rasilimali za kijenetiki.[6]

Kulingana na Ibara 47 ya Itifaki ya kulinda aina ya mimea  kwa nchi za SADC, Itifaki hii itaanza kutumika siku 30 baada ya angalau theluthi mbili ya nchi wanachama watakapokuwa wamekubali kuuridhia. Hata hivyo, kuna wasiwasi iwapo Itifaki ya SADC itakuwa na nguvu ya kisheria ya moja kwa moja kwenye nchi husika kutokana na mifumo tofauti ya sasa ya kisheria ambayo nchi wanachama wameitumia tangu uhuru.[7] Ni jambo lisilofikirika kwamba wanachama wa SADC watajifunga kwa hiari kwenye mfumo wa kikanda ambao uko chini ya mamlaka moja, yenye maamuzi yatokayo juu kuja chini, na kibaya zaidi, unaotokana kwa sehemu kubwa na utaratibu usionyumbuka wa UPOV 1991.

Katika muhtasari huu, tunajadili vipengele muhimu vya Itifaki ya Ulinzi wa aina ya mimea kwa nchi za SADC na wasiwasi kutokana na vifungu vyake vya sheria.

# Wasiwasi kuhusu Itifaki ya kulinda aina ya mbegu kwa nchi za SADC

## Utaratibu wa kulinda aina ya mbegu chini ya mamlaka moja

Itifaki inajenga utaratibu wa kulinda aina ya mimea ulio chini ya mamlaka moja kwa nchi wanachama wa SADC ambao wameridhia Itifaki, ambapo Ofisi ya Haki za Wagunduzi Mimea wa kanda ya SADC (PBRO) watakuwa na mamlaka makubwa ya kutoa na kusimamia haki za wagunduzi  kwa niaba ya nchi hizo wanachama. Hii inajumuisha kutoa haki miliki kwa waguduzi wa mimea, kutoa leseni, kubatilisha au kufuta Haki miliki za Wagunduzi, n.k. Malimbikizo ya haki za wagunduzi hivyo kupendelea maombi yote yawe sawa. Hii inamaanisha kwamba iwapo aina ya mmea inayolindwa na mfumo wa kikanda wa kulinda aina ya mimea  ya SADC, aina hiyo hiyo haiwezi tena kulindwa au kupewa haki nyingine chini ya sheria za Taifa, na ili kukwepa ulinzi mara mbili na sheria tofauti zikitumika kwa aina hiyo hiyo ya mmea. Cha kusikitisha, hakuna vifungu mahususi na taratibu za kuwezesha nchi wanachama kupinga matumizi ya Haki za Wagunduzi Mbegu katika nchi yake na hivyo kuzuia taratibu za uhuru wa taifa kujiamulia. Hili ni kosa kubwa sana – kosa ambalo limeshughulikiwa na Itifaki ya kulinda aina mpya ya mimea ya Arusha katika Ibara 4(1). Nchi binafsi ambazo ni wanachama wa SADC watanyimwa haki ya kufanya maamuzi chini ya mamlaka za nchi zao ambayo yana manufaa kwa nchi zao, yanayogusa kiini halisi cha maendeleo ya taifa ya kijamii na uchumi na mikakati ya kupunguza umasikini.

6. Tembelea ACB (2018a) Kuelekea katika sera za kitaifa za kikanda nchini Afrika ambazo zinatambua na kusaidia mifumo ya mbegu za wakulima.  Inapatikana : http://www.acbio.org.za/sites/default/files/documents/Seed_Policies_in_Africa_report_WEB.pdf.
7. Tembelea Munyi, et al. 2016. *Fursa na vitisho vya kuunganisha haki za wafugaji wa mimea Afrika: ARIPO na SADC*. Inapatikana: https://www.euppublishing.com/doi/pdfplus/10.3366/ajicl.2016.0142

## Kutokuwepo kwa Mfumo wa Kipekee wa kulinda aina ya mimea

Itifaki hii yenye mamlaka kutoka sehemu moja – inayotokana na UPOV 1991 – inakiuka kipengele cha Mfumo wa Kipekee wa kulinda aina ya mimea cha Makubaliano ya Vipengele Vinavyohusiana na Biashara na Haki Miliki za Kitaalamu (TRIPS). Hii ni kwa sababu nchi wanachama wa SADC watakaoridhia Itifaki ya kulinda aina ya mimea kwa nchi za SADC, watatakiwa kutumia mfumo ule ule wa kulinda aina ya mimea ambayo ni kandamizi, bila ya kujali viwango vyao tofauti vya maendeleo ya kilimo, kiuchumi na kijamii. Mbinu hii yenye mamlaka moja inachukulia kwamba kinachofanya kazi katika nchi moja kwenye kanda (k.m. Afrika Kusini) kinapaswa kufanya kazi katika nchi nyingine katika kanda hiyo hiyo (k.m. Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo). Itifaki hii haitoi mwanya kwa kubadilisha na kuweka mifumo ambayo inafaa kwa nchi binafsi kutokana na viwango vya maendeleo kwa wanachama wake walio hatarishi zaidi, kwa maana ya nchi zilizo na maendeleo duni zaidi,[8] ili kuwawezesha kushughulikia changamoto zao za mfumo mahususi wa kilimo na kijamii na kiuchumi.

Wanachama wa SADC ambao ni nchi zilizo na maendeleo duni kwa mujibu wa Shirika la Biashara Duniani, kwa sasa hawalazimiki kutekeleza masharti ya Makubaliano ya TRIPS pamoja na masharti yanayolazimisha ulinzi wa aina za mimea. Wengi wa wanachama hawa wana uzoefu mdogo au hawana kabisa na Mifumo ya kulinda aina ya mimea. Ni athari gani zinaweza kutokea kwa utaratibu huu wa kulinda aina ya mimea usionyumbufu katika uzalishaji wa umma, kwenye ubunifu wa taasisi za utafiti za umma na wakulima na kwenye usalama wa chakula na lishe?

## Kulindwa kwa (jenera na spishi)/ aina yote ya mimea

Itifaki inakwenda zaidi ya masharti ya UPOV 1991 kwa kuruhusu ulinzi wa aina ya mimea kwa (jenera na spishi) mimea aina yote, wakati hata UPOV 1991 hutoa muda wa mpito kwa ulinzi wa mimea. Ukichukulia kwamba Haki za Wagunduzi wa Mimea ni dhana mpya katika kanda, ikiwa na athari zisizojulikana, haileti maana kuweka ulinzi kwa aina yote ya mazao. Unyumbufu ni muhimu ili kuruhusu nchi kuamua ni aina gani ya mimea zijumuishwe na zipi ziondolewe kutoka wigo wa sheria ya ulinzi wa aina ya mimea. Aidha, haki za wagunduzi wa mimea huwa na manufaa zaidi zikihusika kwa mazao ya biashara pekee, hivyo ni muhimu kwa viwango vya ulinzi wa aina ya mimea kutofautishwa kati ya makundi tofauti ya mazao, kama vile mazao ya biashara ambayo sio chakula na mazao ya chakula, ili kuhakikisha usawa katika mifumo ya chakula na mbegu ya ndani. Kwa mfano, nchi mwanachama anaweza akataka kuziondoa aina za mimea ya asili kutoka kwenye ulinzi wa aina ya mimea ili kulinda dhidi ya matumizi mabaya, umiliki binafsi na kwa ujumla, kumomonyoka kwa uanuwai wa kijenetiki na kutengwa kwa aina za asili na mifumo ya mbegu inayosimamiwa na mkulima.

## Kigezo cha NDUS

Kuna maoni kuwa vigezo vya ulinzi wa aina ya mimea/vigezo vinavyotumika kumpa haki miliki mgunduzi kwa maana ya, mpya, za upekee, mfanano na uthabiti (NDUS) zinapuuza aina ya mimea na mbegu za asili za wakulima wadogo. Maoni ni kwamba kutengwa huku na kutotambulika kwa aina za asili za mbegu na mimea ya wakulima, moja kwa moja kunawatenga wakulima kutoka kwenye tafsiri ya 'mgunduzi' kwenye Itifaki, na hii, matokeo yake inazuia aina hizi za mimea na mbegu zisipate ulinzi.[9] Wasiwasi ni kwamba SADC imechagua kufuata mbinu ambayo si sahihi ya UPOV 1991, ambayo huhimiza kuweka viwango na kuondoa uanuwai kwa misingi ya vigezo vya NDUS, badala ya kuendeleza Muundo wa kisheria ambao unaleta faida katika bioanuwai ya kilimo na unaohimiza wakulima kutegemea uanuwai wa mazao,

8. Nchi zenye maendeleo duni katika SADC: Angola, Democratic Republic of Congo (DRC), Lesotho, Madagascar, Malawi, Mozambique, Tanzania na Zambia.
9. Tembelea Correa et al. (2015) *Ulinzi wa aina ya mimea kwa nchi zinazoendelea: Kifaa cha kuandaa mfumo wa ulinzi wa aina ya mimea ya kipekee: Njia mbadala ya UPOV 1991.* Inapatikana: http://www.apbrebes.org/files/seeds/ToolEnglishcompleteDez15.pdf.

jambo ambalo ni muhimu kulinda riziki ya wakulima wakati ambao kuna changamoto ya kukabiliana na tishio linaloibuka la mabadiliko ya tabianchi na za usalama wa chakula zinazokabili kanda. Kinadharia, ulinzi wa aina ya mimea unaweza kuwanufaisha wakulima kwa kulinda aina zao anuwai za mimea dhidi ya uharamia wa kibaiolojia.[10] Kwa bahati mbaya, pamoja na masharti ya NDUS, kuna uwezekano hili lisiwezekane kwa wakulima. Aidha, kutuma maombi ya ulinzi wa aina ya mimea itakuwa ghali na vigumu kwa wakulima kumudu, au hata kampuni ndogo za mbegu. Hii ni kwa sababu mifumo ya ulinzi wa aina ya mimea ina gharama kubwa zinazohusiana na majaribio na uthibitisho kwa ajili ya NDUS. Hili lazima lizingatiwe na Nchi Zilizo na Maendeleo Duni ndani ya SADC, hivyo kuibua mjadala kuhusu ulinzi jumuishi na kutambulika kwa aina za mimea za wakulima—jambo ambalo linapaswa kushughulikiwa katika sera jumuishi ya mifumo ya mbegu inayosimamiwa na wakulima.

Kubaini uasilia wa aina ya mimea [Sub]
Kutokana na shinikizo kutoka Asasi za Kiraia, Itifaki ya ulinzi wa aina ya mimea kwa nchi za SADC inajumuisha, kama sehemu ya masharti ya maombi ya kupata hati ya Haki ya Mgunduzi wa Mimea, tamko kutoka kwa mgunduzi kwamba rasilimali za kijenetiki au rasilimali kutoka kwa mbegu mama vilivyotumika kwa ajili ya kuzalisha, kubadilisha au kuendeleza aina ya mmea vilipatikana kisheria. Masharti haya yanalenga katika kuzuia kuporwa na matumizi mabaya ya rasilimali za kijenetiki, ambayo ni maboresho kwenye rasimu iliyopita ambapo hapakuwepo na kipengele hicho. Hata hivyo, bado haitoi haki ya kugawana manufaa kutokana na matumizi ya rasilimali za kijenetiki ambazo zinaweza kuwa zimepatikana kutoka kwa wakulima na jamii za asili. Hivyo basi Itifaki hii inashindwa kuunga mkono malengo na masharti ya Mkataba wa Bioanuwai (CBD) na Itifaki ya Nagoya ya Kushirikishana Manufaa na Mkataba wa Kimataifa wa Rasilimali za Kijenetiki za Mimea kwa Chakula na Kilimo (ITPGRFA). Ni muhimu sheria ya ulinzi wa aina ya mimea, pamoja na sheria na kanuni zilizoundwa kutekeleza Mikataba ya ITPGRFA, CBD na Nagoya zinaungana mkono na kuendeleza vifungu kuhusu maswala haya nyeti.

## Wigo wa haki za wagunduzi

Ibara ya 27 ya Itifaki ya ulinzi wa aina ya mimea kwa Nchi za SADC imeweka na kupanua haki zilizotolewa kwa wagunduzi kiasi ya kwamba zinafanana na zile zinazotolewa chini ya sheria za hataza (patents). Ibara ya 27 inaainisha kuwa vitendo vinavyohusiana na uzalishaji au kuzalisha, matayarisho kwa madhumuni ya kusambaza, kuuza, au shughuli za masoko, kuuza nje ya nchi, kuagiza kutoka nje, na kuweka hifadhi na kwa madhumuni yoyote yaliyotajwa, yatahitaji ruhusa ya wagunduzi (Ibara 27(1). Ruhusa hii, inaweza kuambatanishwa na masharti na ukomo wa vitendo (Ibara 27(2). Aidha, Ibara 27(3) inaeleza kuwa matumizi ya mavuno yanayotokana na mbegu/ mimea zilizolindwa yatahitaji ruhusa ya mgunduzi isipokuwa tu pale ambapo mhusika amekuwa na fursa ya kutosha ya kutumia haki yake kuhusiana na mmea/ mbegu anayomiliki. Ibara 27(4) inaainisha kuwa masharti yote yaliyotajwa katika Itifaki yatajikita katika aina za mimea yanayotokana na yale yaliyopewa haki miliki (Essentially Derived Varieties). Katika mfumo wa UPOV wa awali, UPOV 1978, masharti ya kuhifadhi, matumizi ya kurudia na kubadilishana miongoni mwa wakulima kwa madhumuni yasiyo ya kibiashara hayajazuiliwa kwa uwazi. Hata hivyo, haki hizi zinaweza kuruhusiwa kwa mkulima kama zinaangukia katika mianya iliyoainishwa chini ya Ibara 28 ya Itifaki ya ulinzi wa aina ya mimea kwa nchi za SADC, kwa mujibu wa masharti kadhaa. Kuhusiana na mavuno kama ilivyotamkwa chini ya Ibara 27(3) ieleweke kwamba UPOV 1978 haihitaji kuendeleza masharti kwenye mavuno au bidhaa nyingine zinazopelekwa sokoni, isipokuwa tu kwa mimea ya mapambo (ornamental plants) ambayo hutumika kwa madhumuni ya uzalishaji. Hata hivyo, Itifaki ya ulinzi wa aina ya mimea kwa nchi za SADC, kuhusiana na mavuno

10. Temebelea ACB (2018) *Kuelekea katika sera za kitaifa za kikanda nchini Afrika ambazo zinatambua na kusaidia mifumo ya mbegu za wakulima*. Inapatikana:http://www.acbio.org.za/sites/default/files/documents/Seed_Policies_in_Africa_report_WEB.pdf

haina masharti makali sana ukilinganisha na Itifaki ya ulinzi wa aina mpya ya mimea ya Arusha ambayo imepanua masharti hata kwa mavuno, isipokuwa tu pale ambapo mgunduzi amekuwa na fursa ya kutosha ya kutumia haki miliki yake kuhusiana na mmea anaotaka kuzalisha kama ilivyoainishwa katika Ibara 27(4) ya Itifaki ya Arusha.[11] Kwa kupanua ulinzi hadi katika aina za mimea muhimu kupitia vipengele chini ya Ibara 27(4), (5) na (6), Itifaki inaweka mazuio makubwa kwenye uwezo wa wakulima kutumia kwa uhuru aina zilizolindwa kwa ajili ya madhumuni ya utafiti na uzalishaji, hivyo kuzuia maendeleo ya aina mpya kutokana na aina zilizolindwa – hususani kwa wakulima wanaozalisha na kutohoa aina za mimea kwa ajili ya mazingira yao, kwa kuchagua.

## Misamaha katika haki za wagunduzi na fursa kufanikisha haki za wakulima

Masharti yanayohusika na mianya katika haki za wagunduzi ni muhimu sana. Ila je, ni kwa kiasi gani misamaha hii inashindwa kufikia haki za wakulima kama zinavyotambulika katika Ibara 9 ya Mkataba wa Kimataifa wa Ulinzi wa Rasilimali za Kijenetiki (ITPGRFA) ambao nchi za Angola, Botswana, Jamhuri wa Kidemokrasi ya Kongo, Eswatini, Lesotho, Madagascar, Mauritius, Malawi, Msumbiji, Namibia, Seychelles, Afrika Kusini, Tanzania, Zambia na Zimbabwe wameridhia?[12] Katika Itifaki ya SADC, misamaha ya haki za wagunduzi inahusiana na vitendo anavyofanya mkulima kwa 'madhumuni ya binafsi na yasiyo ya kibiashara' ambayo kulingana na UPOV 1991 ni msamaha wa lazima. Msamaha wa hiari kwa mujibu wa UPOV 1991 ni ile inayoitwa 'Upendeleo kwa mkulima' kuhusiana na "vitendo vinavyofanywa na mkulima kuhifadhi, kutumia kama mbegu, na kurudia kutumia au kubadilishana kwa madhumuni yasiyo ya kibiashara mavuno yake, ikijumuisha mbegu za mimea iliyolindwa ikizingatia ukomo unaofaa, na kutegemea maslahi halali ya mmiliki wa haki za wagunduzi".[13]

Matumizi ya neno 'binafsi na isiyo ya kibiashara' inaweza kumaanisha matumizi ya aina zilizolindwa kwa ajili ya wakulima wadogo pekee. Hata hivyo, UPOV 1991 inatafsiri 'binafsi na isiyo ya kibiashara' katika maana finyu. Kutokana na hilo, mazoea kama vile kubadilishana, kuuza mbegu za ziada katika soko la ndani la nafaka haiwezi kuchukuliwa kuwa ndani ya mipaka ya matumizi 'binafsi na yasiyo ya kibiashara' isipokuwa kufanya vitendo hivi vinaweza haramu katika nchi za SADC.[14] Hususani, kushirikiana na kubadilishana mbegu zilizolindwa zilizohifadhiwa kutoka shambani miongoni mwa wakulima wadogo ndio msingi wa mifumo ya kilimo kwa Waafrika ambayo hukakikisha uhakika wa chakula na uhifadhi wa mbegu hivyo kuna haja ya kupanua mwanya wa matumizi 'binafsi na yasiyo yakibiashara' sio tu kwa wakulima wote masikini[15] bali kwa wakulima wote wadogo. Tafsiri ya mkulima mdogo inatofautiana kati ya nchi na nchi, na inaweza isiwezekana kwa mfumo wa ulinzi wa aina ya mimea wa kanda kutoa tafsiri hii. Kazi hii iwekwe mikononi mwa nchi binafsi katika sheria zao za kitaifa za ulinzi wa aina ya mimea, baada ya mashauriano na wakulima wadogo na wadau wengine katika nchi zao husika.

Inapokuja katika tafsiri ya kile kinachoitwa 'Upendeleo kwa mkulima' kulingana na Ibara 28 (d) ya Itifaki ya SADC, mambo mengi yatategemea jinsi "madhumuni

11. Kutokana na Ibara 22 na 23, vitendo vilivyotajwa katika aya (1) Vifungu (a) to (g), kwa mujibu wa: ... (b) bidhaa zinazotokana moja kwa moja kwa mavuno ya aina ya mmea uliolindwa ikiwemo ndani ya vipengele vya aya ya (a).
12. Tazama orodha ya wanachama wa ITPGRFA: http://www.fao.org/planttreaty/countries/membership/en/?page=1&ipp=20&no_cache=1&tx_dynalist_pi1[par]=YToxOntzOjE6IkwiO3M6MToiMCI7fQ.
13. Haki za wagunduzi hazitaenea kwa "vitendo vya wakulima wadogo kwa matumizi ya kuzalisha, katika mashamba yao, bidhaa itokanayo na mavuno waliopata kwa ajili ya kupanda, ya mbegu iliyolindwa the protected variety of varieties iliyoainishwa katika Ibara 26(3)(a)(i) au (ii) ya Itifaki hii. Tazama Ibara 27(d) ya Rasimu ya Itifaki ya SADC 2012: http://www.ip-watch.org/weblog/wp-content/uploads/2013/04/SADC-Draft-PVP-Protocol-April-2013.pdf.
14. Tembelea De Jonge, B. 2014. Ulinzi wa aina ya mimea Kusini mwa Jangwa la Sahara: Uwiano kati ya maslahi ya kibiashara na wakulima wadogo. Inapatikana: https://www.researchgate.net/publication/272802664_Plant_Variety_Protection_in_Sub-Saharan_Africa_Balancing_Commercial_and_Smallholder_Farmers'_Interest
15. Tembelea ACB, 2018b. Itifaki na Kanuni za Arusha: Kutaasisisha Muungano wa Kulinda Aina za Mimea(UPOV 1991) katika Mifumo na Sheria za Mbegu za Afrika. https://acbio.org.za/sites/default/files/documents/The%20Arusha%20Protocol%20and%20Regulations_Institutionalising%20UPOV%201991%20in%20African%20seed%20systems%20and%20laws%20Summary.pdf

yasiyo ya kibiashara", "ukomo unaofaa" na "kutegemea maslahi halali ya mmiliki wa haki za wagunduzi" yatakavyo fafanuliwa/ kutafsiriwa zaidi. Kwa upande mmoja, "madhumuni yasiyo ya kibiashara" lazima ifafanuliwe kwa uwazi kiasi kwamba haizuii haki za wakulima. Kwa upande mwingine, "ukomo unaofaa" na "maslahi halali ya mmilik wa haki za mgunduzi" yanapaswa kutafsiriwa ili yasizuie wigo wa matumizi ya rasilimali zilizolindwa na pia kuwapa msamaha wakulima wadogo katika kulipa mrahaba. "Madhumuni yasiyo ya kibiashara" yapewe tafsiri pana, ili wakulima wadogo wawe na uhuru kamili wanapotumia aina ya mbegu/mimea zilizolindwa, pamoja na haki ya kubadilishana na kuuza mbegu na vipandikizi.

# Hitimisho na Mapendekezo

### Kuzingatia tofauti baina ya Itifaki za Ulinzi wa mimea za SADC na Arusha

Nchi nyingi wanachama wa SADC (zaidi ya nusu) ni wanachama wa ARIPO. Nchi wanachama wa SADC ambao ni wanachama wa ARIPO na SADC watakabiliwa na mapungufu yaliyomo kwenye masharti ya misamaha kwa haki za wagunduzi baina ya Itifaki zote mbili.[16] Hii inaweza kusababisha kuchanganyikiwa kuhusu Itifaki ipi kati ya hizi mbili inafaa kuridhiwa, kutokana na tofauti kubwa kati ya masharti ya Itifaki hizo.

**Masuala ya Uhuru wa taifa kujiamulia**

Kama ilivyotamkwa hapo awali, kitu cha kutia wasiwasi katika Itifaki ya ulinzi wa aina ya mimea kwa nchi za SADC ni kwamba Itifaki haitoi nafasi yoyote kwa nchi zilizoridhia kupinga kikanda kwa kutolewa kwa Haki za Wagunduzi wa Mimea katika nchi zao, kama ilivyotamkwa katika Itifaki ya Arusha. Kwa vile Itifaki tayari imesharidhiwa, itakuwa vigumu sana kurekebisha upungufu huu. Je, kanuni za Itifaki ya ulinzi wa aina ya mimea kwa nchi za SADC zinaweza kurekebisha upungufu huu?

**Kubaini asilia**

Hitaji la kuthibitisha kwamba rasilimali za kijenetiki zimepatikana kisheria na kubainisha chanzo cha rasilimali ni hatua muhimu dhidi ya matumizi mabaya/ uharamia wa rasilimali za kijenetiki. Masharti haya hayajajumuishwa katika Itifaki ya ulinzi wa aina ya mimea ya Arusha. Hata hivyo, Itifaki ya SADC haiendi mbali sana, kwani haihitaji wakulima kushiriki katika kugawana faida. Je, kanuni zinaweza kurekebisha upungufu huu na kufanya Itifaki iendane na sheria za nchi za kugawana manufaa katika ngazi ya taifa?

**Misamaha katika haki za wagunduzi**

Misamaha ya haki za wagunduzi katika Itifaki ya ulinzi wa aina ya mimea kwa nchi za SADC inaruhusu wakulima kujumuisha vitendo vinavyofanywa na mkulima kwa madhumuni "binafsi na yasiyo ya kibiashara" na vitendo vinavyofanywa na mkulima "kuhifadhi, kutumia, kupanda, kurudia kupanda na kubadilishana mbegu zilizohifadhiwa kutoka shambani na vipandikizi vingine vya aina za mbegu zilizolindwa –kutegemea ukomo unaofaa na kulinda maslahi ya mgunduzi.

Itifaki ya ulinzi wa aina ya mimea ya Arusha inatoa masharti ya mianya michache tu kwa makundi mahususi ya wakulima na hutegemea orodha ya mazao ya kilimo na mboga mboga yaliyoainishwa na Baraza la Utawala na yanayohusishwa na mazoea ya kihistoria ya kuhifadhi mbegu katika nchi zilizoridhia kwa matumizi ya uzalishaji na abidhaa zilizovunwa katika shamba la mkulima mwenyewe. Orodha hii haihusishi matunda, mzao ya mapambo (ornamentals), aina za mboga mboga na miti ya msituni.[17] Aidha, hii bado itahusisha malipo ya mrahaba kwa wakulima wadogo na wakulima wakubwa wa kibiashara.[18] Hii inaonyesha kwamba mianya hii inahusu wakulima wadogo tu ambao watasamehewa kulipa mirahaba. Hata hivyo, wakulima wadogo wa kibiashara watakuwa katika hasara kiuchumi ukilinganisha na wale wa Ulaya kwani watatakiwa kulipa mirahaba kwa wagunduzi.

16. Tafadhali rejea Kiambatisho na Mukhtasari wa ripoti ya ACB Tafadhali rejea kwenye orodha ya marejeo ya ripoti kamili
17. Tazama Ibara 22(2) ya Itifaki ya Arusha ya Ulinzi wa aina ya mimea.
18. Tazama Ibara 22(3) ya Itifaki ya Arusha ya Ulinzi wa aina ya mimea.

Je, kanuni za kutekeleza Itifaki ya ulinzi wa aina ya mimea kwa nchi za SADC zitatumia tafsiri pana kwa "binafsi na yasiyo ya kibiashara", (ii) 'ukomo unaofaa' na (iii) 'kulinda maslahi ya mgunduzi'?.

Wakati tunapinga kwa dhati mifumo inayohodhi mamlaka ya ulinzi wa aina ya mimea unaotokana na UPOV 1991, tunapendekeza iwapo kanuni za kutekeleza Itifaki ya SADC zitatungwa, basi zitekeleze haki za wakulima na sio kuzuia shughuli yoyote ya mkulima zinazohusiana na matumizi ya aina ya mimea/mbegu zilizolindwa. Hii itahitaji tafsiri stahiki ya neno 'mkulima' ijumuishe wakulima wadogo na wakulima wadogo wa kibiashara ambao hawatatakiwa kulipa mirahaba kwa wagunduzi. Kunaweza pakawa na tofauti ya wazi na tafsiri ya makundi tofauti ya wakulima ndani ya kanda ya SADC, kama vile wakulima wadogo, wakulima wadogo wa kibiashara na wakulima wakubwa wa kibiashara kwa vigezo vya ukubwa wa mashamba yaliyolimwa, aina ya mazao yaliyopandwa, jumla ya kipato au faida kutokana na mauzo ya mbegu/mazao kwa mwaka, na kadhalika, na kulingana na makubaliano kupitia mashauriano na nchi wanachama, kwani vipengele hivi hutofautiana kutoka nchi moja kwenda nyingine. Katika orodha ya maoni yaliyowasilishwa ARIPO kuhusiana na rasimu ya kanuni, Asasi za Kiraia za Afrika zimesisitiza kwamba hata Umoja wa Ulaya (EU) inawasamehe wakulima wadogo (pamoja na wakulima wadogo wa kibiashara) kulipa mirahaba kwa kuhifadhi na kurudia kutumia mbegu na kuzizalisha katika mashamba yao wenyewe pale ambapo mbegu hizo na vipandikizi hutokana na aina za mbegu zilizoorodheshwa kuwa zimelindwa. Matokeo yake ni kwamba wakulima wa ulaya wapo katika hali nzuri zaidi kiuchumi kuliko wakulima wa Kiafrika. Itakuwa ni jambo la uonevu mkubwa na lisilo la uadilifu na kumuweka mkulima mdogo wa kibiashara wa Afrika katika fursa mbaya zaidi kuliko wakulima wenzake wa Kizungu ambao ni matajiri zaidi. Angalau wakulima wa kiafrika wapate msamaha wa kulipa mirahaba, kama ilivyo katika Umoja wa Ulaya.

Hivyo, kuna haja ya kuwa na uwazi na ushirikishwaji wakutosha katika kutengeneza kanuni za ulinzi wa aina ya mimea za SADC kwa ajili ya utekelezaji wa Itifaki hio. Mchakato huu wa kutunga sera unatakiwa uwe jumuishi wa wadau wote wahusika wakiwemo wakulima wa Kiafrika na asasi za kiraia, na zihusishe milolongo ya mashauriano sahihi ili kukuza mchakato wakufanya maamuzi usiopendelea upande wowote, kabla na baada ya rasimu ya kanuni kuandikwa na kuidhinishwa.

## Mapendekezo kwa nchi wanachama wa SADC

Kutokana na masuala yaliyoangaziwa katika Itifaki ya SADC, hususani utaratibu wa ulinzi wa aina ya mimea ulio kandamizi na usionyambufu, na unaohodhi mamlaka unaotokana na UPOV 1991, tunazitaka nchi wanachama wasiridhie Itifaki ya ulinzi wa aina ya mimea ya SADC. Katika chapisho tofauti, tumetoa hoja inayofanana kwa nini nchi wanachama wa SADC, vilevile na wa ARIPO wasiridhie Itifaki ya ulinzi ya aina ya mimea ya ARIPO.

Nchi zenye maendeleo duni ndani ya SADC watumie fursa ya muda ulioongezwa—kama ilivyoainishwa katika makubaliano ya TRIPS—kuandaa mifumo ya ulinzi ya aina ya mimea inayofaa na yenye unyumbufu, ambayo inatoa haki sawa kwa haki za wagunduzi na haki za wakulima, na hii itategemea kinachofanyika hadi mwisho wa muda ulioongezwa Kwa nchi za Afrika zilizo ndani ya Makubaliano ya TRIPS, TRIPS inatoa mnyambuko kwa ajili ya kuandaa mfumo wa kipekee kushughulikia maslahi ya taifa na mifumo ya kilimo. Mifumo ya kipekee kama hiyo inaweza kukidhi masharti ya Shirika la Biashara Duniani, pia na kuhakikisha utaratibu wa haki wa mbegu, tofauti na viwango vya UPOV ambayo tayari ni mfumo wa kulazimisha usawa iliyoundwa kukidhi masoko yaliyoendelezwa ya mbegu ya Ulaya na biashara ya kilimo. Kwa mfano, nchi za India na Malaysia wameunda mifumo yao ya kipekee ya ulinzi wa aina ya mimea ambayo ni sikivu kwa mazingira yao ya kilimo.[19]

19. Tembelea (2015) *Plant variety protection in developing countries: A tool for designing a sui generis plant variety protection system: An alternative to UPOV 1991.* Inapatikana: http://www.apbrebes.org/files/seeds/ToolEnglishcompleteDez15.pdf.

Kwa zile nchi ambazo ni lazima kuweka sheria za ulinzi wa aina ya mimea, tunapendekeza yafuatayo:

- Kila nchi ifanye tathmini huru iliyo shirikishi ili kupima athari za mfumo wa ulinzi wa aina ya mimea uliokusudiwa kwa wakulima wadogo na jamii kwa ujumla. Izingatiwe kwamba UPOV 1991 inaleta tishio katika kufikia na kufurahia haki za binadamu, hususani haki ya kupata chakula, kupitia katazo la matumizi, kubadilishana na kuuziana mbegu, ambazo ukijumuisha bei za juu na zinazoendelea kupanda na kushuka kwa kipato cha kaya inaweza kuathiri upatikanaji wa chakula, huduma za afya na elimu.[20] Hivyo, tathmini hiyo lazima izingatie heshima na ulinzi wa haki za binadamu, ambayo ni pamoja na haki ya kupata chakula, kipato na uanuwai wa mazao.
- Majadiliano ya kutosha yanahitaji kufanyika na wadau wahusika ambao ni pamoja na wakulima wadogo wa Kiafrika, jamii za wenyeji na Asasi za Kiraia. Hii ihusishe mlolongo wa midahalo na mashauriano ya umma, kwa kuzingatia matokeo ya utafiti wa athari za mifumo ya ulinzi wa aina ya mimea.
- Nchi wanachama zihakikishe kwamba majukumu yao chini ya mikataba ya Kimataifa ikijumuisha CBD, ITPGRA na Itifaki ya Nagoya kuhusu Upatikanaji na Kugawana Manufaa, pia na mikataba mbalimbali ya kulinda haki za binadamu, zinaakisiwa katika sheria zao za ulinzi wa aina ya mimea, hususani kuhusiana na utekelezaji wa haki za wakulima na ulinzi dhidi ya uharamia wa bioanuwai.

20. Tembelea Berne Declaration et al. (2015) *Kumiliki mbegu, kufikia chakula: Tathmini ya athari za haki za binadamu ya ulinzi wa aina ya mimea*. Inapatikana: https://www.publiceye.ch/fileadmin/files/documents/Handelspolitik/Factsheet_2015_01_DB_HRIA_UPOV_EN.pdf

# Kiambatisho

## Kulinganisha kati ya Itifaki ya ulinzi wa aina ya mimea za SADC na Arusha (ARIPO)

| | Itifaki ya SADC | Itifaki ya Arusha (ARIPO) |
|---|---|---|
| Kuidhinisha na kuridhia | Iliridhiwa na Mkutano wa 37 wa Wakuu wa Nchi na Serikali za SADC mjini Pretoria, Afrika Kusini mnamo tarehe 19 n a 20 Agosti 2017.<br><br>Kanuni hazijaundwa hadi leo developed to date. | Itifaki iliridhiwa na Mkutano wa Kidiplomasia ARIPO mjini Arusha, Tanzania, Julai 2015.<br><br>Kanuni ziliridhiwa na Baraza la Utawala la ARIPO nchini Malawi, Novemba 2017. |
| Waliotia saini | Angola, Congo DRC, Zambia, Eswatini na Namibia. | Ghana, Gambia, Msumbiji, São Tomé na Príncipe, na Tanzania. |
| Itakapoanza kutumika | Wakati theluthi mbili wanaporidhia Itifaki. | Wakati nchi nne zinaporidhia. Hakuna nchi iliyoridhia. |
| Nchi wanachama | Nchi 16 wanachama: Angola, Botswana, Comoros, Congo DRC , Eswatini, Lesotho, Madagascar, Malawi, Msumbiji, Namibia, Seychelles, Afrika Kusini, Tanzania, Zambia, Zimbabwe. | Nchi 19 wanachama: Botswana, Gambia, Ghana, Kenya, Eswatini, Lesotho, Malawi, Msumbiji, Namibia, Sierra Leone, Liberia, Rwanda, São Tomé and Príncipe, Somalia, Sudan, Tanzania, Uganda, Zambia na Zimbabwe. |
| Nchi wanachama | 9 | 13 |
| Nchi wanachama ambao ni wanachama wa ITPGRFA | 11 | 14 |
| Pingamizi | Hakuna kifungu kinachowezesha nchi wanachama kupinga Haki za Wagunduzi wa Mimea kutumika katika nchi zao.<br><br>Pingamizi ya awali la mtu yeyote litolewe ndani ya siku 60 baada ya maombi ya haki ya mgunduzi kufanywa (Ibara 22(2)). | Ibara 4(1) ya Itifaki na Sheria 12 ya kanuni inaruhusu kutoa zabuni ili kupinga haki ya mgunduzi kutumika katika nchi zake, ndani ya miezi 6 kutoka tarehe ambayo maombi ya haki miliki ya ugunduzi wa mbegu yalifanyika.<br><br>Inatoa miezi 3 kwa pingamizi ya awali kufanyika (Ibara 16).<br><br>Ada ya Dola 250 kwa pingamizi (kanuni 5(2)).<br><br>Maamuzi ya kuzuia Haki miliki ugunduzi wa mbegu katika nchi yanahitaji kuhalalishwa kwenye ofisi za haki miliki za ARIPO (Kanuni 12(1) (a)(iii)). |

| | Itifaki ya SADC | Itifaki ya Arusha (ARIPO) |
|---|---|---|
| NDUS: Upekee wa NDUS | Aina ya mmea lazima iweze kutofautishwa wazi kabisa kutoka kwenye aina yoyote ya mmea ambayo tayari inatambulika *popote duniani*. Aidha, Ibara 9(2) inaweka kwa muhtasari vigezo kuhusu aina ya mmea ambayo tayari inatambulika kama vile:<br>• Matumizi ya vipandikizi au mavuno ya aina ya mmea tayari yamekuwepo sokoni kwa madhumuni ya kibiashara;<br>• Aina ya mmea ipo katika orodha rasmi au daftari la aina ya mimea katika nchi yoyote mwanachama wa SADC au nje ya kanda ya SADC au imeelezewa kwa kiundani katika chapisho lolote la kitaalamu; au<br>• Kujumuishwa kwa aina katika mkusanyiko wa aina za mimea ambazo zinapatikana/kifikiwa na umma. Kujumuishwa kwa aina katika mkusanyiko wa aina za mimea lazima ijumuishe matukio ambayo si lazima yajulikane kwa umma. | Iweze kutambulika wazi utofauti wake na aina nyingine ambao uwepo wake ni maarifa ya kawaida wakati wowote wa kutuma maombi.<br><br>Hakuna tafsiri ya aina ya mimea ambayo 'tayari inatambulika' |
| Muda wa ulinzi | Miaka 25 kwa miti na mizabibu na miaka 20 kwa aina nyingine za mimea (jenera na spishi). Inaelezea zaidi kwamba Baraza la Ushauri linaweza kuongeza muda hadi miaka mitano (hiari ni miaka 5), hivyo kwenda zaidi ya UPOV 1991. | Miaka 25 kwa miti na mizabibu na miaka 20 kwa aina nyingine za mimea (jenera na spishi). (Ibara 26). |

| | Itifaki ya SADC | Itifaki ya Arusha (ARIPO) |
|---|---|---|
| Mianya | Ibara 28(d) Vitendo vinavyofanywa na mkulima kuhifadhi, kutumia, kupanda na kurudia kupanda au kubadilishana kwa matumizi yasiyo ya kibiashara, ya mavuno shambani ikijumuisha mbegu za aina inayolindwa, ndani ya mipaka inayofaa na kulinda maslahi halali ya mwenye haki ya mzalishaji. | Ibara 22(2) Mwanya pekee kwa mkulima unaoruhusiwa na Itifaki ni kwa mazao ya kilimo yaliyoainishwa na Baraza la Utawala kwa masharti kwamba mrahaba unalipwa na mkulima kwa mgunduzi.<br><br>Matunda, maua, mboga mboga zimeondolewa kutoka katika wigo wa mianya ya Itifaki.<br>Ibara 22(3) Masharti ya utekelezaji wa vipengele chini ya aya (2), kama vile ngazi tofauti za mirahaba kulipwa na wakulima wadogo wa kibiashara na wakulima wakubwa wa kibiashara na taarifa itakayotolewa na mkulima kwa mgunduzi, itaainishwa kwenye kanuni. |
| Kubaini asilia | Inahitaji tamko kwamba mbegu asilia/rasilimali za kijenetiki zilipatikana kwa njia halali (Ibara 13(5)(e)), lakini haihakikishi kufuatwa kwa makubaliano haya na mengine ya kimataifa. | Haijaweka kipengele chochote au utaratibu kuhakikisha upatikanaji kihalali wa rasilimali za kijenetiki. |
| Ulinzi wa aina za mimea zilizopo | Ibara 40 inaruhusu kutolewa kwa haki miliki ya wagunduzi kwa aina zilizopo kwa kuzingatia siku zilizopita, hata kama hazikidhi kigezo cha upya. | Hakuna kipengele |

Chanzo: ACBb. Tafadhali rejea kwenye orodha ya marejeo ya ripoti kamili

| | ARIPO | SADC | ITPGRFA | UPOV member (1978 or 1991) | WTO member | Least developed country designation | National PBRs law in place |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Angola | | • | • | | • | • | |
| Botswana | • | • | | | • | | |
| Comoros | | • | | •* | | • | |
| DR Congo | | • | • | | • | • | |
| Djibouti | | | • | | • | • | |
| Eswatini | • | • | • | | • | | |
| Gambia | • | | | | • | • | |
| Ghana | • | | • | | • | | |
| Kenya | • | | • | •*** | • | | • |
| Lesotho | • | • | • | | • | • | |
| Liberia | • | | • | | | • | |
| Madagascar | | • | • | | • | • | |
| Malawi | • | • | • | | • | • | |
| Mauritius | | • | • | | • | | |
| Mozambique | • | • | | | • | • | • |
| Namibia | • | • | • | | • | | |
| Rwanda | • | | • | | • | • | • |
| Sao Tome & Principe | • | | • | | | • | |
| Sierra Leone | | • | • | | • | • | |
| Somalia | • | | | | | • | |
| South Africa | | • | | •** | • | | • |
| Sudan | • | | • | | | • | |
| Tanzania | • | • | • | •*** | • | • | • |
| Uganda | • | | • | | • | • | • |
| Zambia | • | • | • | | • | • | • |
| Zimbabwe | • | • | • | | • | | • |
| **Total** | 18 | 16 | 20 | 4 | 21 | 18 | 8 |

* through the African Intellectual Property Organization (OAPI) ** UPOV 1978 *** UPOV 1991

Adapted from Munyi et al., 2016

african centre for biodiversity

PO Box 29170, Melville 2109, South Africa
www.acbio.org.za